JAMUHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA
OFISI YA RAISI- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKARI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA (M)
SHULE YA SEKONDARI SONGEA BOYS
S. L. P. 2, SONGEA. Simu: (+255) 766089787/0769336999 Email: contact@songeaboys.ac.tz

2024-22-11

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI SONGEA BOYS -2025

Natumia nafasi hii kukupongeza kwa kufanya vizuri mtihani wa darasa la saba. Hivyo Kwa barua hii ninakujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha KWANZA katika shule ya sekondari ya Songea Boys, ambayo ni ya bweni kwa wavulana tu. Shule hii ipo katika mji wa Songea, Mkoa wa Ruvuma, umbali wa kilometa sita (06) kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa barabara ya Tunduru.

Shule itafungua tarehe 04/01/2024 na mwisho wa kuripoti shuleni ni siku ishirini (20) mara baada ya tarehe ya kufungua yaani tarehe 24/01/2024, ukichelewa hautapokelewa. Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo:

i. **Form namba 1 Fomu ya afya (requesting for medical examination). Apimwe hospitali na mganga mkuu wa wilaya/ mkoa kuhusu afya yake, udanganyifu hautavumiliwa.**
ii. **Form namba 2 Orodha ya mahitaji ya muhimu ya shule**
iii. **Form namba 3 Kukubali/ Kukataa nafasi uliyochaguliwa katika shule ya Songea Boys**
iv. **Form namba 4 Sheria za shule.**

Tafadhali, soma kwa makini kabla wewe na mzazi/mlezi wako hamjazijaza fomu hizo. Kumbuka kuwa kila mwanafunzi anapaswa kujaza fomu zote kikamilifu na kuzirejesha hapa siku atakayo ripoti. Bila kukamilisha taratibu zote zilizoandikwa (matakwa ya usajili) HAUTOPOKELEWA. Mwisho ninakukaribisha na kukutakia mafanikio mema hapa shuleni kupitia NIDHAMU, MAARIFA na JUHUDI.

Ahasante

The Headmaster
Songea Boys Secondary School
Songea

LUGOME G.
MKUU WA SHULE

JAMUHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA
OFISI YA RAISI- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKARI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA (M)
SHULE YA SEKONDARI SONGEA BOYS
S. L. P. 2, SONGEA. Simu: (+255) 766089787/0769336999 Email: contact@songeaboys.ac.tz

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION
To be completed by a medical officer:

Student's Full name……

Age: ……. Years; sex: ……..…

Blood count (red and white) ……..……..…

Stool examination: ……..……

Urine analysis: ……

Eye test: ……. ……..

T.B test: ……..……

Ears: ……

Chest: ……..……..

Spleen: ……..…

Abdomen: ……..……

ADDITIONAL INFORMATION e.g. Physical defects or important infections, chronic of family diseases, etc.
……
……
……
……
……
……
……
……
I certify that the above named candidate is fit to pursue his studies.
Medical Officer's Names: ……
Designation: ……Signature: ……
Station: …… Date: ……..……

NOTE:
Medical Officer: At the time of examination of the particular student for any ailment please note
Student: You must bring this completed form at registration time, none of you may enroll without certificate of physical fitness.

FOMU NA: 2 FOMU YA MAHITAJI YA SHULE
SARE ZA SHULE

1. Suruali mbili nyeusi zishonwe kwa unadhifu na ziwe na LINDA pia mkunjo (turn up) **(inaweza kushonwa shuleni kwa Tsh. 22,000/= kila moja)**
2. Shati nyeupe mbili za mikono mifupi. Mashati yatawekwa michoro ya utambulisho hapa Shuleni. Mashati lazima yawe na kola shingoni**, (unaweza yapata kwenye duka lililoko shuleni)**
3. Fulana ya shule – Zinaweza kupatikana shuleni kwa Tsh 15,000/= (hizi huwekwa nembo ya shule na kuwa sare rasmi atokapo nje ya shule)
4. Viatu vyeusi vya ngozi, soksi nyeusi jozi mbili ama zaidi
5. **Kofia za duara** kwa wale wenye ulemavu wa ngozi (albinism)
6. Sweta rangi ya bluu lenye nembo ya shule, **linaweza kupatikana shuleni kwa Tsh.20,000/=**.
7. Nguo za michezo –bukta nyekundu, fulana ya kijani na raba nyekundu au nyeusi **zinaweza patikana shuleni**.
8. Tracksuit ya bluu- bahari (light blue) **zinaweza patikana shuleni kwa Tsh. 20,000/=**.
9. Nguo za kazi – kaptura ya kaki (Tsh.18,000/=) na fulana ya kijani. Nguo hizi lazima zivaliwe wakati wa kazi (**zinaweza kushonwa shuleni**

NB: (NGUO NYINGINEZO HAZIRUHUSIWI)

MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI

Ingawa mahitaji haya ni ya mwanafunzi binafsi, yanatakiwa kuwasillishwa kwenye ofisi ya mkuu wa shule siku ya kuwasili ili yakaguliwe na taratibu nyingine utafahamishwa.

VIFAA VYA DARASANI (kadili ya aina ya tahasusi njoo na matini mbalimbali-wasiliana na mwalimu wa taaluma MS. Anaida Mwambeleko-0767577164 kwa ufafanuzi zaidi)

1. Daftari za kutosha angalau ishirini (12) (i.e. Msomi)
2. Counter books angalau kumi na tano (12)
3. Kalamu za kutosha
4. Mkebe (Mathematical set)
5. Stop Watch, sio saa janja (smart watch)
6. Limu moja kwaajili ya majaribio

VIFAA VYA BWENINI

1. Ndoo moja na lita 10
2. Sabuni za kufulia na kuogea za kutosha
3. Godoro (ft 2 ½)- 1
4. Mto na foronya (Rangi foronya ifanane na rangi ya shuka)
5. Mashuka (2) ya rangi ya Light Blue na blanketi (1)

6. Chandarua cha mstatiri cha rangi ya BLUU-(1)
7. Mafuta ya kujipaka
8. Dawa za meno na miswaki
9. Nguo za ndani (vest na chupi za kutosha)

VIFAA VYA BWALONI

1. Kikombe -(1)
2. Sahani-(1)
3. Bakuri-(1)
4. Kijiko-(1)

N.B 1:

Aje na fedha za kumtosha kwa ajili ya matumizi yake binafsi akiwa hapa shuleni. **Unashauriwa ajiunge na bima ya afya hapa shuleni ambayo gharama yake ni Tsh. 50,400/= kwa mwaka, KAMA HANA. Ikumbukwe suala la afya ni nyeti katika kujifunza, haswa kwa mtoto huyu aliyeko mbali na wazazi.**

NB 2:

ILI KUONDOA USUMBUFU WA KUSAFIRI NA MIZIGO: VIFAA NA MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA MWANAFUNZI VINAAPATIKANA KATIKA DUKA LILIKO SHULENI, TUMEAMBATANISHA BEI ZA MAHITAJI YANAYOPATIKANA HAPA CHINI:

FOMU NA: 3

JAMUHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA
OFISI YA RAISI- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKARI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA (M)
SHULE YA SEKONDARI SONGEA BOYS
S. L. P. 2, SONGEA. Simu: (+255) 766089787/0769336999 Email: contact@songeaboys.ac.tz

YAH: KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2025

Mimi .....……..... ninakujulisha kuwa NIMEKUBALI/ NIMEKATAA (**kata isiyo husika**) KUJIUNGA NA SHULE YA SONGEA BOYS. Hii ni baada ya majadiliono na mzazi/mlezi wangu, tumekubaliana kuwa nitazifuata sheria za shule kama zilivyo ainishwa na kwamba endapo nitakaidi kufuata taratibu za shule basi hatua za nidhamu zichukuliwe dhidi yangu. KWA ALIYEKATAA NAFASI: Baada ya majadiliano na mzazi/mlezi wangu tumekubaliana kuwa nafasi hiyo hatuitaki na kwamba itolewe kwa mwanafunzi mwingine wa AKIBA.

JINA LA MWANAFUNZI: ..... SAINI YA MWANAFUNZI.....
JINA LA MZAZI/MLEZI..... SAINI YA MZAZI/MLEZI.....
TAREHE: …….....

TAARIFA ZA MWANAFUNZI
Jina la mwanafunzi..... Namba ya Cheti cha kuzaliwa ……
Tarehe ya kuzaliwa..... Mahali alipo zaliwa (wilaya)..... (Mkoa).....
(Kama sio Mtanzania ambatanisha nakala zinazokutambulisha kutoka ofisi za uhamiaji nchini). Dini.....
Dhehebu.....

TAARIFA ZA MZAZI/ MLEZI
Jina la mzazi/mlezi anaye kutunza..... Namba ya NIDA……...
Kazi ya Mzazi/Mlezi..... Kiwango cha Elimu ……..……
Anuani/simu ya mzazi/Mlezi..... Uhusiano na Mwanafunzi.....
Mahali anapoishi Mzazi/Mlezi - Kijiji/mtaa: …….……..……..……Kata.....

MAJINA YA NDUGU WENGINE WAWILI WANAO HUSIKA NA MALEZI YA MWANAFUNZI
Ndugu: ..... Anuani yake:.....
Namba ya simu: .....

Ndugu: ..... Anuani yake: .....
Namba ya simu: .....

TAARIFA ZA SERIKALI YA KIJIJI/ MTAA ATOKAKO MWANAFUNZI
Jina la mtendaji wa kata..... Kata ya .....…
Anuani.....… Namba ya simu.....
Sahihi na Muhuli ……..
Jina la Mwenyekiti wa mtaa/ kijiji..... .... Kijiji/mtaa cha/wa .....
Anuani.....… Namba ya simu.....

FOMU NA:4 SHERIA ZA SHULE

Shule ni mahali ambapo mwanfunzi hujipatia elimu kwa mategemeo ya kujitayarisha kwa maisha yake ya sasa na baade. Anategemea kutumia uwezo wote kujiendeleza kielimu (maarifa ya kukabiliana na mazingira) kinidhamu, utii na vile vile kuishi vizuri katika jamii ndani na nje ya shule. Ili kuhakikisha kuwa lengo hilo linafanikiwa, SHERIA ZA SHULE zimewekwa. Sheria hizi ni muhimu kwa sababu zina jukumu kubwa la kulinda haki, thamani, utu wa kila mwanafunzi na sifa nzuri ya shule na tunu za taifa. Walimu na wafanyakazi wasio walimu wote ni viongozi na walezi wa wanafunzi shuleni. Kila mmoja anawajibu wa kuhakikisha kuwa maisha ya kila mwanafunzi yanakuwa mazuri na yenye furaha sawa shuleni na badae. Nia ya shule ni kujenga nidhamu, maarifa na juhudi; busara ya kushika madaraka, kutii sheria na kutovunja ahadi, ushirikiano na hisani kisha kumuendeleza kitaluuma kila mwanafunzi darasani na nje ya mipaka ya shule. Shule itamlea kila mwanafunzi na kumkuza katika misingi ya jamii katika hali yake ya uhuru, utu, usawa na kuthamini wengine katika jamii yake ndani na nje ya shule. Ili kumpatia mwanafunzi misingi hiyo katika maisha yake ya baade, anapaswa kuzingatia sheria za shule kama ifuatavyo: -

1. Kila mwanafunzi anapaswa kutumia akili zake za asili na busara katika kufanya uamuzi wa vitendo mbalimbali shuleni na nje ya shule.
2. KUWAHI:
    i. Kila mwanfunzi anapaswa kuwahi kuamka asubuhi na kufanya usafi wa mazingira na mahali anapolala pia kuwahi kwenye paredi saa 1:00 asubuhi hivyo kuchelewa ni kosa.
    ii. Kila mwanafunzi anapaswa kuwahi kwenye eneo la paredi “Assembly ground” kila inapogongwa kengele Kila mwanafunzi lazima awahi (kukimbia) anapoitwa na kiongozi (mwalimu, mfanyakazi au kiranja)
3. HESHIMA
   Wanafunzi wanapaswa kuheshimiana wenyewe na kumheshimu mtu yeyote anapokutana naye au kumkuta sehemu yoyote.
4. UTORO
   Ni kosa kwa mwanafunzi kutoroka shule/ darasani wakati ule anapokuwa shuleni/darasani kwa hiyo asitoke nje ya shule bila kibali (ruhusa)toka kwa mwalimu wa zamu/ uongozi wa shule.
5. SIMU
   Simu haziruhusiwi na nikosa kwa mwanafunzi kumiliki simu au kutumia simu pasipo ruhusa. Simu zote zikabidhiwe kwa mkuu wa shule pindi mwanafunzi anapofika shuleni- atarejeshewa siku ya kufunga/ kuhitimu shule.
6. UTUNZAJI WA VIFAA VYA SHULE
   Ni kosa kwa mwanafunzi yeyote kuharibu mali ya shule kwa kukusudia kama vile; vitabu, viti, madawati, miundo mbinu ya umeme, vifaa vya maabara n.k UNUNUZI WA KIFAA KIPYA/ FIDIO LA GHARAMA ZA MATENGENEZO vitakuwa ndiyo adhabu ya awali.
7. WIZI
   Ni kosa kwa mwanafunzi kuiba kushiriki katika kitendo cha wizi hata kikiwa kidogo.
8. UTULIVU NA AMANI
    i. Ni kosa kwa mwanafunzi kupiga kelele akiwa darasani au hata nje ya darasa katika mazingira ya shule.
    ii. Ni kosa kwa wanafunzi kugombana au kuchochea ili wengine wagombane.
    iii. Ni kosa kwa wanafunzi kufanya mgomo au kushiriki katika aina yeyote ya mgomo.
    iv. Kazi ni wajibu wa kila mwanafunzi, kwa hiyo ni kosa kwa mwanafunzi kutofanya au kutegea kazi za mikono ambazo zitakuwa zimepangwa na viongozi ama walezi wako (wafanyakazi wa Songea Boys).
9. TAALUMA;
   NI kosa kubwa kwa mwanafunzi, kutohudhuria vipindi na kutofanya mitihani ya ndani (terminal test, quiz n.k) na mazoezi yoyote yatolewayo na walimu wa masomo darasani.
10. ULEVI NA UVUTAJI
    i. Ni kosa kwa mwanafunzi kuvuta /kuuza sigara, bangi na kunywa aina yoyote ya pombe.

ii. Ni kosa kwa mwanafunzi kuonekana akizurula kwenye maeneo ya nyumba za wageni (guest houses), mabaa ya pombe ama kumbi za starehe (night clubs).

11. UASHERATI
    Ni kosa mwanafunzi kujihusisha na vitendo vya uasherati na iwapo mwanafunzi atabainika kuwezesha ama kushiriki vitendo vya uasherati basi atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe.
12. MIPAKA YA MWANAFUNZI
    Ni kosa kwa mwanafunzi kuonekana kwenye nyumba za walimu au wafanyakazi wasio waalimu bila ruhusa ya mkuu wa shule. Lakini pia ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya eneo la shule pasipo kibali cha kufanya hivyo (Kibali hicho kitatolewa na mwalimu wa zamu ama ofisi ya mkuu wa shule).
13. UTU NA THAMANI YA SHULE
    Ni kosa na marufuku kwa mwanafunzi kufanya vitendo viovu vinavyoweza kudhalilisha ama kushusha heshima na kuleta sifa mbaya kwako binafsi, kwa mwanafunzi mwenzako na kwa shule.

N.B: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI;

i. Wizi.
ii. Uasherati, ubakaji na ushoga.
iii. Ulevi, uvutaji wa bangi na matumizi ya madawa ya kulevya.
iv. Makosa yoyote jinai.
v. Kupiga au kupigana.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma /shule
vii. Kudharau bendera ya taifa.
viii. Kushiriki kutoa mimba.
ix. Kugoma, kuchochea mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
x. Kukataa adhabu kwa makusudi.
xi. Kukutwa na simu ya mkononi.
xii. Kutowajibika kitaaluma

LUGOME G.
MKUU WA SHULE